# TACOMA

### KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA

Kima cha chini cha mshahara kwa mwaka 2019 eneo la Tacoma ni $12.35 kwa saa.

# SEATAC

## VIWANGO MAHUSUSI KWA TASNIA

Ikiwa unafanya kazi katika **hoteli kubwa** (zaidi ya vyumba 100) au **kazi inayohusiana na uwanja wa ndege** katika Jiji la SeaTac -- ikiwemo huduma nyingi za vyakula, uuzaji wa rejareja, mashirika ya kukodisha magari pamoja na maegesho -- una haki zifuatazo kazini.

### KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA

Kima cha chini cha mshahara kwa wanaofanya kazi katika hoteli kubwa na huduma nyingine za uwanja wa ndege jijini SeaTac ni $16.09 kwa saa kwa mwaka 2019.

### KUHIMIZA AJIRA YA MUDA MREFU

Mwajiri wako lazima awape wafanyakazi waliopo saa za ziada za kazi kabla ya kuajiri wafanyakazi wengine au kutafuta mkadarasi wa ziada.

# JIMBO ZIMA

### KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA

Kima cha chini na mshahara katika eneo la Washington ni $11.50 kwa saa na inatumika kwa kazi zote, ikiwemo kilimoa, kwa wafanyakazi wote walio na miaka 16 na zaidi.

- Mwajiri wako sharti akulipe bakshishi zote unazopokea
- Bahashishi halali za pamoja haziwezi kujumuisha mmiliki, meneja, au msimamizi
- Pia ni lazima ulipwe ada zote za huduma zinazoongezwa kwenye bili za wateja, isipokuwa kama bili imetaja vinginevyo
- Mwajiri wako hawezi kukulipa kiwango kilichopungua kima cha chini cha mshahara ili kusawazisha na malipo unayopata kutokana na bakshishi au ada za huduma

### LIKIZO YA KUUGUA NA USALAMA YENYE MALIPO

Waajiri wote Washington sharti wawapatie wafanyakazi wao muda wa likizo ya kuugua na usalama yenye malipo. Kwa kila saa 40 ambazo mwajiriwa anafanya kazi, sharti apate angalau saa 1 ya likizo. Unaweza kutumia muda wa kuruhusiwa kutokuja kazini unapokuwa mgonjwa huku ukilipwa wakati wewe au mtu fulani katika familia au boma yako anahitaji:

- Kwenda kwa daktari
- Kuuguzwa baada ya maradhi
- Kushughulikia masuala yanayohusu migogoro ya ndoa, ukatili wa kijinsia au uviziaji

### FURSA SAWA YA KUAJIRIWA

Katika mchakato wa kuajiri, mwajiri HAFAI:

- Tangaza nafasi za kazi ambazo hazijumuishi watu ambao waliwahi kukamatwa na polisi au kupatikana na hatia kortini
- Jumuisha swali lolote kwenye barua ya kuomba kazi ukiuliza rekodi za kukamatwa na polisi au kupatikana na hatia kortini
- Ulizia kuhusu rekodi yako hadi mwajiri aamue kuwa vinginevyo unafaa kwa kazi

Sheria hii haitumiki kwa kazi za kutekeleza sheria au ulinzi, taasisi za kifedha, wala kwa kazi zinazohitaji utunzaji usio na usimamizi wa watu walio hatarini.

**FAIR WORK**
**CENTER**

Kituo cha Usawa Kazini huwezesha wafanyakazi kupata usawa kazini. Sisi ni kitovu cha wafanyakazi kuelewa na kutekeleza haki zao za kisheria, kuboresha hali za kazi na kuungana na rasilimali za jamii.

Tunatazamia kuwepo na jamii ambapo wafanyakazi wanashughulikiwa kwa hadhi na heshima, bila kuzingatia tabakai, jinsia, au mbari. Tutafanya kazi ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wamefahamu haki zao chini ya sheria na kwamba waajiri wanawajibikia viwango vya kazi.

Kituo cha Usawa Kazini hutoa usaidizi ufuatao kwa wafanyakazi:

- Tunatoa rasilimali zinazoeleza haki za waajiriwa katika lugha tofauti
- Tunafanya warsha za kuhamasisha kuhusu haki zako na usalama na afya kazini kwa lugha tofauti
- Tunawasaidia wafanyakazi kufahamu mashirika ya mji, jimbo, na serikali kuu
- Tunatoa ushauri wa kisheria bila malipo kwa wafanyakazi wanaotafuta nasaha kuhusu uwezekano wa kukiukwa kwa haki kazini

# WASILIANA NASI

*Una maswali kuhusu haki zako kazini?*
*Unataka kuratibu mkutano wa Zifahamu Haki Zako?*


**1-844-485-1195**

**help@fairworkcenter.org**

**www.fairworkcenter.org**

**116 Warren Ave N, Suite A**
**Seattle, WA 9819**


# FAHAMU HAKI ZAKO KAZINI

## 2019

**FAIR WORK**
**CENTER**

SWAHILI

# SEATTLE

**Ikiwa unafanya kazi Seattle, una haki za ziada kazini. Kumbuka: Chini ya sheria za Seattle ni kinyume cha sheria kwa mwajiri wako kulipiza kisasi dhidi yako kwa kuuliza au kutekeleza hali zako.**

## *KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA*

Sheria hii haitumiki kwa kazi za kutekeleza sheria au ulinzi, taasisi za kifedha, wala kwa kazi zinazohitaji utunzaji usio na usimamizi wa watu walio hatarini.

| Waajiri Wakubwa (Waajiriwa 501+) |
|---|
| **$16.00/saa** |

| Waajiri Wadogo (Waajiriwa 500 au chini) | |
|---|---|
| **Je, wewe hupokea $3/saa kama bahashishi na/au manufaa ya matibabu?** | |
| **Hapana: $15.00/saa** | **Ndiyo: $12.00/saa** |

## *WIZI WA MSHAHARA*

Wizi wa mshahara ni pale ambapo mwajiri wako anapokosa kukulipa kwa kazi yote uliyofanya. Mifano ya wizi wa mshahara ni pamoja na UNAPOKOSA:

- Kulipwa kima cha chini cha mshahara
- Kulipwa kiwango ulichoahidiwa
- Kulipwa muda wa iada uliofanya kazi
- Mapumziko ya dakika 10 yenye malipo

Vilevile, unapoajiriwa mwajiri wako sharti akupe taarifa iliyoandikwa inayojumuisha maelezo kuhusu anwani ya mawasiliano, kiasi cha ujiwa wako na siku za kulipwa.

## *LIKIZO YA KUUGUA NA USALAMA YENYE MALIPO*

Ikiwa unafanya kazi Seattle unastahiki kulipwa kwa muda unapokuwa katika likizo ya kuugua na usalama iwe unafanya kazi muda wote, kwa muda kidogo au kazi isiyo ya kudumu. Muda unaolipwa unategemea mwajiri wako:

| Mwajiri ana wafanyakazi **250 au zaidi**: | Mwajiri ana wafanyakazi **wasiozidi 250**: |
|---|---|
| Unapokea **saa 1 kwa kila saa 30** ulizofanya kazi | Unapokea **saa 1 kwa kila saa 40** ulizofanya kazi |

Unaweza kutumia muda wa kuruhusiwa kutokuja kazini unapokuwa mgonjwa huku ukilipwa wakati wewe au mtu fulani katika familia au boma yako anahitaji:

- Kwenda kwa daktari
- Kuuguzwa baada ya maradhi
- Kushughulikia masuala yanayohusu migogoro ya ndoa, ukatili wa kijinsia au uviziaji

## *FURSA SAWA YA KUAJIRIWA*

Katika mchakato wa kuajiri, mwajiri HAFAI:

- Kutoa tangazo la kazi linalosema hufai kuomba kazi ikiwa una rekodi ya kuwahi kushikwa au kuhukumiwa
- Kuuliza maswali kuhusu rekodi yako mpaka baada ya kuwachuja waombaji wengine ambao hawakutimiza masharti

Mwajiri sharti akupe nafasi ya kufafanua kuhusu au kusahihisha rekodi yako.

Ikiwa mwajiri hatakupa kazi kwa sababu ya rekodi yako, ni sharti sababu hiyo uhusiane na wewe kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi au mwajiri lazima ataje sababu halali za kibishara.

Sheria hii haitumiki katika kazi za kutekeleza sheria au ulinzi au kazi zinazohusu kuwalinda watu wanaohitaji usaidizi.

## *VIWANGO MAHUSUSI KWA TASNIA*

### *WAFANYAKAZI WA HUDUMA ZA VYAKULA NA UUZAJI: URATIBU SALAMA*

Ikiwa unafanya kazi kwa muuzaji mkubwa wa bidhaa za rejareja au vyakula vya haraka (zaidi ya wafanyakazi 500) au mgahawa ulio na matawi kote nchini, mwajiri wako SHARTI:

- Atoe ratiba yako ya kazi mapema kwa siku 14
- Akupe malipo ya ziada kwa kubadilisha ratiba iliyokuwa imechapishwa (isipokuwa kama umeomba kubadilishiwa zamu)
- Akuruhusu ukatae zamu za kufunga na kufungua kazi zilizo na kipindi kisichozidi saa 10 kati yazo, au akulipe zaidi kwa kufanya zamu hizo
- Awape wafanyakazi waliopo saa za ziada za kazi kabla ya kuajiri wafanyakazi wengine
- Ukupe kadirio la jumla ya saa za kazi unazofaa kutarajia kufanya kazi wakati unaajiriwa

### *WAFANYAKAZI WA HOTELI: MIKAKATI YA AFYA NA USALAMA*

Ikiwa unafanya kazi katika hoteli ya Seattle iliyo na zaidi ya vyumba 60, mwajiri wako SHARTI:

- Akupe vitufe vya kubofya ukiwa na hofu na mbinu nyingine za kujikinga dhidi ya ukatili na mashambulizi ya kijinsia
- Akuruhusu kuendelea kuwa an kazi yako usimamizi wa hoteli unapobadilika

***Hoteli Kubwa (zaidi ya vyumba 100)***

- Kutoa mafao ya kimatibabu na fidia nyinginezo (huenda isitumike katika hali zote)
- Kuwapa watunzaji wa nyumba malipo zaidi kwa kuosha zaidi ya futi 5,000 za mraba katika zamu ya saa 8 (takriban vyumba 15 vya kawaida)

### *SHERIA YA HAKI ZA WAFANYAKAZI WA NYUMBANI*

Kuanzia tarehe 1 Julai, ikiwa wewe ni mfanyakazi wa nyumbani – ama kama mwajiriwa na mkandarasi huru – **anayefanya kazi katika nyumba za watu kama yaya, mwoshaji nyumba, mfanyakazi wa utunzaji wa nyumba, mfanyakazi wa kupalilia shamba, mpishi, na/au meneja wa boma**, una haki zifuatazo chini ya sheria mpya:

- Malipo ya Kiwango cha Chini Zaidi cha Ujira cha Seattle
- Mapumziko mafupi ya mfululizo wa dakika 30 ya kupata maakuli ikiwa unafanya kazi kwa zaidi ya saa tano kwenye boma moja
- Mapumziko mafupi ya mfululizo wa dakika 10 kwa kila saa nne unazofanya kazi kwenye boma moja
- Ikiwa haiwezekani uwe na mapumziko ya kupata maakuli, mwajiri wako ni lazima akupe malipo ya ziada kwa ajili ya mapumziko hayo uliyokosa
- Ikiwa wewe ni mtunzaji asiyeenda nyumbani baada ya kazi kila siku, ni lazima uwe na siku moja ya mapumziko baada ya kufanya kazi kwa siku sita mfululizo
- Mwajiri wako haruhusiwi kuweka vitu au hati zozote zako za kibinafsi kama vile pasipoti au visa
- Huunda Bodi ya Viwango vya Kazi inayowashirikisha wafanyakazi ili kutekeleza na kupanua haki hizi

***UNA MASWALI KUHUSU HAKI ZAKO KAZINI? TUPIGIE SIMU: 1-844-485-1195***